# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA (MB), WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA TATU (3) CHA SERIKALI MTANDAO, FEBRUARI 10, 2023 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.

---

Mhe. Felician Mtahengerwa; Mkuu wa Wilaya ya Arusha,

Bw. Xavier Daudi; Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,

Dkt. Jasmine Tiisekwa, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Makatibu Tawala wa Mikoa,

Wajumbe wa BODI ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Mhandisi. Benedict Ndomba, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Mkurugenzi Mkuu Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

Wakuu wa Idara za Tehama na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali;

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana;

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

***Serikali Mtandao …… Pamoja Tunatekeleza***

Ndugu Washiriki, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wote kwa ushiriki wenu mzuri katika Kikao Kazi hiki cha 3 cha Serikali Mtandao, ambacho tunakihitimisha leo. Nipende tu kusema kuwa, nimefarijika kwa namna mlivyoshiriki kwa ukamilifu katika majadiliano, pamoja na kutoa maoni na ushauri katika masuala mbalimbali yaliyowasilishwa yenye lengo la kuimarisha na kukuza

utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma.

Kipekee kabisa, nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), kwa ushiriki wake katika Kikao Kazi hiki. Vilevile, naipongeza Kamati ya Maandalizi kwa mada nzuri zilizotoa uelewa mkubwa kuhusu hali na mipango ya utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao, pamoja na huduma nzuri wakati wote wa kikao.

Aidha, nawashukuru Watoa Mada, pamoja na waendesha majadiliano wote kwa uwasilishaji mzuri wa mada pamoja na uendeshaji wa mijadala uliosheheni weledi na umahiri wa hali ya juu katika eneo la Serikali Mtandao. Mada hizo zimekuwa chachu na msingi wa majadiliano kwa muda wa siku zote tatu mlizokuwa hapa. Si jambo jepesi kuwakusanya watu wote hawa na kuwafanya wafurahie uwasilishaji wa mada na kushiriki kikamilifu katika majadiliano, niseme tena hongereni sana.

Ndugu Washiriki, Kama ilivyoelezwa wakati wa ufunguzi wa Kikao Kazi hiki tarehe 8 Februari, 2023, kuwa Kikao hiki kililenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, ili kujadiliana hali ya utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao na kuweka mikakati ya namna bora ya kuziendeleza, pamoja na kuainisha changamoto na kuziwekea mikakati madhubuti ya kukabiliana nazo.

Ndugu Washiriki, Kikao hiki kimekuwa na mafanikio makubwa sana, kwanza kimewakutanisha washiriki zaidi ya 1,624 wa kada tofauti Kutoka katika Taasisi mbalimbali za umma. Mchanganyiko huu umesaidia kupata maoni na ushauri mbadala kuhusu utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao zinazolenga kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma.

Ndugu washiriki, kupitia kikao hiki jumla ya mada 22 zinazohusu Serikali Mtandao zimewasilishwa. Nimefurahi zaidi kuona wawasilishaji wa mada hizo wanatoka katika

maeneo yote, kwa maana ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na taasisi nyingine za umma. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, Serikali Mtandao imekuwa nyenzo wezeshi sio tu katika kuboresha utendaji kazi wa taasisi hizi, bali pia katika utoaji wa huduma kwa umma, na kuhakikisha wanafikiwa wote, kuanzia waliopo mijini hadi wale wa vijijini, ambapo Wizara kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao imejipanga kuhakikisha upatikanaji wa mifumo ambayo ni rahisi kutumika kwa wananchi wote.

Ndugu Washiriki, nina imani kuwa, sote tunahitimisha Kikao hiki tukiwa na uelewa sahihi na kwa mpana zaidi kuhusu wajibu wetu kama Viongozi na Watumishi katika taasisi za umma katika kuhakikisha kuwa tunazingatia Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, Kanuni zake, pamoja na miongozo na viwango vya Serikali Mtandao iliyoidhinishwa, ili kuwa tunakuwa na matumizi salama na sahihi TEHAMA.

Ndugu Washiriki, Kutokana na umuhimu wa Taasisi za Umma kubadilishana taarifa, nina imani kuwa baada ya

kutamatika kwa Kikao Kazi hiki, Taasisi zote ambazo bado hazijajiunga na Mfumo wa kubadilishana taarifa serikalini (Gov-ESB) zitafanya hivyo, ili kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa baina ya Taasisi za Umma na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Ndugu Washiriki, pamoja na jitihada ambazo Mamlaka ya Serikali Mtandao inaendelea kuzitekeleza hususan za kupunguza urudufu wa Mifumo, ni matarajio yangu kuwa, wataalamu wetu wa TEHAMA katika Taasisi zenu wataendelea kushirikiana na Mamlaka katika Kusanifu na kujenga Mifumo mbalimbali, pamoja na kutekeleza jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao kulingana na mahitaji yaliyopo.

Ndugu Washiriki; Kupitia Kikao Kazi hiki, mmepata fursa pia ya kukumbushwa kuhusu wajibu na nafasi ya kila mmoja wetu, pamoja na Maafisa Masuuli katika kuweka mazingira mazuri na wezeshi ya kufanikisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Nina imani kuwa, kila afisa TEHAMA aliyeshiriki kikao kazi hiki amefahamu nafasi

yake katika kutekeleza jitihada hizo, hivyo nawasihi tukaweke uzalendo mbele kwa kufanya kazi kwa pamoja na kwa uadilifu, wala asitokee mtu akafanya hujuma ili kukwamisha au kurudisha nyumba mafanikio yaliyopatika katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.

Ndugu Washiriki; Napenda kuwahakikishia kuwa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeyapokea maoni yote mliyoyatoa kupitia kikao hiki na inaahidi kuyafanyia kazi na kuweka mpango kazi maalum kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wake. Pia, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kisera na kisheria kuiwezesha Mamlaka kuendelea kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao.

Ndugu Washiriki; Napenda kusisitiza kuwa, maazimo mbalimbali yaliyofikiwa kupitia Kikao Kazi hiki hayana budi kutekelezwa kikamilifu, kwani ili tuweze kuyafikia malengo ya kuwa na Serikali ya Kidijiti kwa asilimia mia moja ni lazima sote kama viongozi na watendaji katika

taasisi za umma tujitume kwa dhati na kufanya kazi kwa uadilifu na ushirikiano wa kutosha.

Kuhitimika kwa kikao kazi hiki ni mwanzo wa maandalizi ya kikao kazi kijacho, hivyo niwaase kuzingatia yote tuliyoazimia, ili katika kikao kazi kijacho tuwe katika nafasi nzuri ya kupima utekelezaji wake kabla ya kuazimia mambo mengine makubwa zaidi yanayoendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, pamoja na kutimiza mahitaji ya kufikia Mapinduzi ya 4 ya Viwanda.

Ndugu Washiriki; Baada ya kueleza hayo, natamka kuwa, Kikao Kazi cha Tatu (3) cha Serikali Mtandao kimefungwa rasmi, niwatakie safari njema mnaporejea katika vituo vyenu vya kazi na karibuni tena wakati mwingine tutakapowaalika.

***Serikali Mtandao …… Pamoja Tunatekeleza***

MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI AFRIKA

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA